



# Dhuluma ya Mahari (Dowry Abuse)

## Mzozo au unyanyasaji unaohusiana na mahari ni aina ya mzozo wa nyumbani na wa kifamilia.

Tamaduni za mahari zinaweza kutofautiana kutoka nchi na tamaduni moja hadi nyingine.

'Mahari' ni desturi inayorejelea pesa, mali au zawadi ambazo kwa kawaida hupeanwa na familia ya mwanamke kwa mume wake baada ya kufunga ndoa. Matumizi ya mahari kivyake si aina ya dhuluma.

Kitendo chochote cha kushurutisha, mzozo au unyanyasaji unaohusiana na kutoa au kupokea mahari wakati wowote kabla, wakati au baada ya ndoa ni aina ya dhuluma. Dhuluma inayohusiana na mahari kwa kawaida huhusisha madai kwamba mahari hayakulipwa na kudai pesa au zawadi zaidi kutoka kwa mwanamke na familia yake.

Mzozo wa nyumbani na wa kifamilia ni uhalifu na ni kinyume cha sheria nchini Australia. Mtu anayetokeleza uhalifu huu anaweza kufungwa jela, awe ni mwanamume au mwanamke.

Ikiwa wewe au mtu unayemjua yuko hatarini, piga simu kwa polisi, nambari ya simu **000**.

Polisi nchini Australia ni salama na wanaweza kuaminika.

Kwa ushauri na maelezo ya bila malipo na ya siri, piga simu kwa 1800RESPECT, nambari ya simu **1800 737 732**.

Ikiwa unahitaji mkalimani bila malipo piga simu kwa **131 450**.

## Serikali ya Australia (Australian Government) haikubali mzozo au unyanyasaji unaohusiana na mahari katika hali yoyote ile.

Serikali ya Australia (Australian Government) huchukulia suala la mzozo wa kifamilia, ikiwa ni pamoja mzozo au unyanyasaji unaohusiana na mahari, kwa uzito sana. Wana-Australia wote wana haki ya kuishi bila mzozo, hofu au kushurutishwa, haijalishi desturi na imani yao ya kidini na kitamaduni.

Mzozo na unyanyasaji unaohusiana na mahari hujumuisha tabia au vitisho ambavyo vinalenga kudhibiti mwenzi au familia yake kwa kusababisha hofu au kutishia usalama wao.

## Ikiwa una visa unaweza bado kupata msaada.

Mwenzi, jamaa au watu wengine katika jamii hawawezi kutishia hali yako ya visa.

Ikiwa unamiliki visa ya muda ya Mwenzi (subclass 309 au 820) au Visa ya Ndoa Inayotarajiwa (subclass 300) na upitie mzozo wa familia unaohusiana na mahari, kuna masharti ya mzozo wa familia katika sheria za uhamiaji za Australia ya kukuwezesha kuendelea na maombi ya visa yako ya kudumu ya Mwenzi (subclass 100 au 801).

## Mahari hayawezi kutumiwa kukulazimisha kuolewa.

Ikiwa mahari yalitumiwa kama njia ya kumlazimisha mtu kuolewa bila idhini yao kamili na huru, hii inaweza kuwa ndoa ya lazima.

Nchini Australia, kila mtu ana uhuru wa kuchagua kama, ni nani, na ni lini anataka kuolewa. Ni kinyume cha sheria ya Australia kumlazimisha, kumtishia au kumlaghai mtu kuolewa. Pia ni kinyume cha sheria kuhimiza au kusaidia kupanga ndoa ya lazima, na kuwa sehemu ya ndoa ya lazima ikiwa wewe ni mhadhiriwa. Hii inatumika kwa ndoa halali, za kitamaduni na za kidini.

## Kuna huduma zinazozingatia utamaduni nchini Australia ambazo zinaweza kukusaidia.

**1800RESPECT** ni huduma ya ushauri wa mzozo wa kijinsia, uhasama wa kifamilia na kinyumbani kutoka kwa taifa la Australia. Hutoa maelezo na ushauri wa mtandaoni na wa simu bila malipo na wa siri. Washauri watakusikiliza, watajibu maswali na kukuelekeza kwa huduma nyingine za msaada katika eneo lako.

Piga simu kwa **1800 737 732** au nenda kwenye **tovuti ya 1800RESPECT** kwenye **[www.1800RESPECT.org.au](http://www.1800RESPECT.org.au)**.

**My Blue Sky** ni tovuti ya kitaifa ya Australia na laini ya msaada iliyotolewa ili kuzuia ndoa za lazima, kutoa maelezo, rufaa na ushauri wa kisheria bila malipo.

Piga simu kwa **(02) 9514 8115**, tuma ujumbe mfupi kwa **0481 070 844**, au utume barua pepe kwa **[help@mybluesky.org.au](mailto:help@mybluesky.org.au)**, au nenda kwenye tovuti ya **My Blue Sky** kwenye **[www.mybluesky.org.au](http://www.mybluesky.org.au)**

Maelezo ya ziada kuhusu mzozo wa kifamilia na visa, ndoa za lazima na biashara haramu ya usafirishaji wa Wanadamu yako kwenye tovuti ya Idara ya Masuala ya Ndani (**Department of Home Affairs**) kwenye **[www.homeaffairs.gov.au](http://www.homeaffairs.gov.au)** na utafute “ndoa za lazima”.

## Je, unahitaji mkalimani?

Piga simu kwa **Huduma ya Ufasiri na Ukalimani (Translating and Interpreting Service (TIS))**, nambari ya simu **131 450**. Mkalimani kutoka TIS anaweza kukusaidia kuwasiliana na huduma zingine, hata hivyo TIS haitoi huduma ya ushauri. Simu zote hazilipishwi na ni za siri.